TANGAZO LA SERIKALI NA. 238 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MWAKITOLYO YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Mwakitolyo ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina kwa eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

*Tangazo la Serikali na. 238 (Linaendelea.)*

———

JEDWALI

———

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*
Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji na namba A yenye majira - nukta 472299.667MS, 9626195.013KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KZ01º01'58.05''MS kwa umbali wa kilomita 1.59 ukikatiza barabara ya Kahama - Shinyanga kupitia Senta ya Burige hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 472270.833MS, 9624595.529KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KS86º32'36.17''MS kwa umbali wa kilometa 1.01 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 471259.918MS, 9624656.591KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KS04º25'07.03''MG kwa umbali wa kilometa 0.37 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 471288.753MS, 9625029.748KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KS78º34'56.77''MS kwa umbali wa kilometa 0.531 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 470768.030MS, 9625134.910KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KZ38º01'54.28''MS kwa umbali wa kilometa 0.217 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 470634.033MS, 9624963.597KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KS89º51'38.14''MS kwa umbali wa kilomita 0.697 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G yenye majira - nukta 469936.909MS, 9624965.293KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KS14º21'31.29''MS kwa umbali wa kilometa 1.67 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H yenye majira - nukta 469646.865MS, 9626098.332KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KS87º54'46.00''MG kwa umbali wa kilometa 2.654 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*